TANGAZO LA SERIKALI NA. 748 la tarehe 16/12/2022

SHERIA YA MWENENDO WA MASHAURI YA JINAI,

(SURA YA 20)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 205A)*

## AMRI YA UTEUZI WA WATAALAMU WA UCHUNGUZI WA SILAHA NA MILIPUKO YA MWAKA 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Uteuzi wa Wataalamu wa Uchunguzi wa Silaha na Milipuko ya Mwaka 2022.

Uteuzi wa wataalamu wa uchunguzi wa silaha na milipuko

2. Watu ambao majina yao yameorodheshwa katika Jedwali wanateuliwa kuwa wataalamu wa uchunguzi wa silaha na milipuko kwa madhumuni ya kutoa taarifa kama ushahidi katika shauri lolote la jinai na masuala mengine yanayohusiana.

Muda wa uteuzi

3.-(1) Muda wa uteuzi utakuwa ni miaka mitano kutoka tarehe ya kuanza kutumika kwa Amri hii.

(2) Bila kujali ujumla wa aya hii, mtu aliyeteuliwa chini ya Amri hii atafanya kazi kwa kipindi chini ya miaka mitano endapo ajira ya mtu huyo itafikia tamati au uteuzi wa mtu huyo utatenguliwa au kusitishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Jina |
|---|---|
| 1. | PF. 17206 SP John Mayunga Sangija |
| 2. | PF. 17913 ASP Paul Methusela Mgema |
| 3. | F. 5914 F/CPL Hafidhi Abdalla Mohamed |
| 4. | H. 4088 F/C Zakayo Joshwa Okejo |
| 5. | H. 4225 F/C Elisha Timoth Mwakajinga |
| 6. | WP. 10462 F/C Julieth Stephano Elisante |
| 7. | WP. 10462 F/C Glory Hassani Ally |

Dodoma,
28 Oktoba, 2022

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU
*Mkurugenzi wa Mashtaka*